JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI).
HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA.

SHULE YA SEKONDARI UBANG'I,
S.L.P 13,
VUCHAMA-UGWENO.
TAREHE 18-12-2020.

KUMB. NA. UBSS/S.2758/KJU/VOL.I/……

JINA LA MWANAFUNZI……

SHULE YA MSINGI……..……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA KUTWA UBANG'I KIDATO CHA KWANZA – 2021.

1. (a) Ninayo furaha kukupongeza na kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga katika shule hii kidato cha kwanza mwaka – 2021.
   (b) Shule hii ipo kata ya Mwaniko, kijiji cha Vuchama, tarafa ya Ugweno, Wilaya ya Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro.
   (c) Shule itafunguliwa rasmi muhula wa kwanza tarehe 11-01-2021, unatakiwa ufike shuleni tarehe hiyo ya kufungua, kwani masomo yataanza mara tu baada ya shule kufunguliwa, baada ya hapo hutapokelewa.
   (d) Tafadhali jaza na kuzirudisha fomu zilizoambatanishwa wakati unaporipoti shuleni. Form ya uthibitisho wa Afya yako (Medical examination sheet) ijazwe na daktari wa wilaya au kituo cha Afya kinachotambulika

2. **Utakaporipoti shuleni hakikisha unaleta vifaa vifuatavyo:**
   (a) VIFAA VYA TAALUMA:
      i. Daftari kumi kubwa, kalamu 5, bluu au nyeusi, penseli na rula ya sentimeta 30.
      ii. Mkebe wa vifaa vya hisabati (mathematical set).
      iii. Four figures (mathematical table).
      iv. Kamusi ya kiingereza (Dictionary).
      v. Picha 2 (passport size) kwa ajili ya jalada la kumbukumbu zako.

   (b) VIFAA VINGINE.
      Unatakiwa uje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya shughuli za usafi.
      (i) **WASICHANA:** Ndoo 1 ya lita 20 na ufagio wa chelewa.
      (ii) **WAVULANA:** Jembe jipya na lenye mpini.

3. **SARE YA SHULE**. **(NUNUA NA UJE UKIWA UMEIVAA SIKU YA KUFUNGUA SHULE)**
   (A) **WASICHANA**. Mashati meupe 2 yenye mikono mifupi, Sketi 2 (ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu, mshono ni rinda box mbele na nyuma) rangi ya DARK BLUE (sampuli imeambatanishwa) au hijab kwa wanafunzi wa Kiislamu (ushungi unaofunika kiwiko cha mkono na nusu kanzu inayofunika makalio), Soksi nyeupe, viatu jozi 2 (vyeusi vya ngozi vinavyofungwa na gidamu na vyenye visigino vifupi).
   (B) **WAVULANA**. Mashati meupe 2 yenye mikono mifupi, Suruali 2 (upana chini usipungue inchi 17 na usizidi inchi 19) rangi ya DARK BLUE (sampuli ya kitambaa imeambatanishwa), soksi, viatu jozi 2 (vyeusi vya ngozi vinavyofungwa na gidamu na vyenye visigino vifupi).

N.B:
HUTAPOKELEWA SHULENI USIPOKAMILISHA VIFAA NA SARE KAMA ILIVYOELEKEZWA.

3.0 <u>SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII.</u>

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi;

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wowote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wowote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wowote.
(i) Kutunza amali za jamii.

3.1 <u>MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUSABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.</u>

(a) Wizi.
(b) Uasherati na ushoga.
(c) Ubakaji.
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kuleva, uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
(e) Kupigana au kupiga.
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(g) Kudharau bendera ya Taifa.
(h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
(i) Kuoa au kuolewa.
(j) Kutoa mimba.
(k) Kugoma, kuchochea au kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama shule.
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(m) Kuwa na simu ya mkononi shuleni.

4.0: CHAKULA CHA MCHANA [**NI LAZIMA KWA WOTE]** KWA MHULA WA KWANZA NI **TSHS. 35,000/= AU MAHINDI DEBE MBILI, MAHARAGE SADOLINI 2 NA TSHS. 15,000/=** [**NI MAKUBALIANO YA KAMATI YA CHAKULA YA WAZAZI NA WAZAZI**]. VYOTE HIVI VITAPOKELEWA NA KAMATI SHULENI SIKU YA KUFUNGUA SHULE.

5.0. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu na pia jaza na kamilisha fomu mbili zilizoambatanishwa [fomu ya taarifa binafsi na utii wa sheria za shule na fomu ya kupima afya ya mwanafunzi].

KARIBU SANA UBANG'I SEKONDARI.

_____
JUMAA E. MSUYA.
MKUU WA SHULE.
Simu. 0655-881085.



SHULE YA SEKONDARI UBANG'I

FOMU YA MAPOKEZI SHULENI.

TAARIFA ZA MWANAFUNZI NA HATI YA KUKUBALIANA NA TARATIBU ZA SHULE.

(FOMU HII IJAZWE NA IRUDISHWE SHULENI SIKU YA KUFUNGUA).

SEHEMU A: (Ijazwe na mwanafunzi)

Jina la mwanafunzi (majina 3)_____

Tarehe ya kuzaliwa_____ Jinsia _____

Kijiji_____Kata _____ Wilaya _____Mkoa _____

Uraia_____ Dini_____

Shule ya msingi utokayo ni_____ Darasa la saba mwaka_____

Nakubali kujiunga na shule ya sekondari UBANG'I na kwamba nitafuata taratibu zote na kinyume na hapo niadhibiwe. SAHIHI YA MWANAFUNZI_____TAR._____

SEHEMU B: (**Ijazwe na mzazi/mlezi anayemsomesha**).

Jina la mzazi/mlezi (majina 3)_____

Anwani yake:_____

Simu _____ mahali anapoishi _____

Kazi anayofanya _____ mahali anapofanyia kazi_____

Nakubali kumpa huduma na kumwendeleza mwanangu na nitashirikana na walimu ili kuhakikisha kuwa anafuata taratibu zote za shule kwa manufaa yake na Taifa kwa mujibu wa kanuni na sheria za shule. SAHIHI YA MZAZI/MLEZI_____ TAR._____

SEHEMU C: HALI YA WAZAZI [Ijazwe na mwanafunzi].

Wazazi wako wote wapo hai [NDIYO/HAPANA] _____

Kama una mzazi mmoja mtaje ni Baba Au Mama _____

Kama hawapo wote ni nani unayemtegemea kukupatia mahitaji yako?

[A] JINA LAKE_____ UHUSIANO_____

[B] ANUANI YAKE; S. L. P_____ SIMU_____

Taja watu wengine wawili wanaoweza kukusaidia.

1. Jina _____ Uhusiano_____

   Anwani_____ Simu _____

2. Jina _____ Uhusiano_____

   Anwani_____ Simu _____

THE PRESIDENT OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT.
MWANGA DISTRICT COUNCIL.
UBANG'I SECONDARY SCHOOL.

TO MEDICAL OFFICER
_____
_____
_____

RE: MEDICAL EXAMINATION.

Pupil's name _____

Please examine the above named pupil as to his/her fitness for this school.

1. Asthma_____
2. Stool examination _____
3. Urine_____
4. T.B_____
5. Leprosy_____
6. Syphilis and other V.D _____
7. Eye test _____
8. Ears _____
9. Epilepsy _____
10. Limbs_____
11. Pregnancy_____
12. Diabetes _____

Additional information eg. Physical defects or impairments, chronic or family disease

(eg. Sickle cell) and others. _____

_____

I certify that the above named student is fit/ is not fit to pursue Secondary Education.

Signature _____ Designation _____ Date _____

OFFICIAL STAMP